**1,150,000>> Idadi ya mifugo iliyopo Halmashauri ya Ikungi**

# Serikali yasema haitawaonea huruma wafugaji watakaokiuka sheria za nchi

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI imewataka wafugaji kote nchini kufahamu nchi yeyote duniani inaendeshwa kwa sheria, utaratibu na kanuni, hivyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, haitamtetea mfugaji yeyote atakayeenda kinyume na sheria kwa kulisha mifugo yake katika eneo au shamba la mmiliki mwingine bila kufuata utaratibu.

Aidha, imesema itahakikisha changamoto ya malisho ya mifugo nchini inatatuliwa kwa wafugaji kuelimishwa namna ya kulima malisho bora yenye tija kwa mifugo yao.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati akikagua shamba darasa la malisho ya mifugo katika Kijiji cha Mahambe, kilichoko Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Mkoani Singida.

"Serikali itaendelea kuwatia moyo wafugaji ili wawe na mashamba ya malisho bora ya mifugo yao na kuhakikisha uwepo wa maji ya kutosha ya kunyweshea mifugo, mambo ambayo yatasaidia kudhibiti migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumaji wengine wa ardhi," alisema.

Aliwataka makatibu tawala wa mikoa mingine, waige mfano wa mkoa wa Singida kwa kuandaa mashamba ya malisho ya mifugo, akisisitiza utaratibu huo uendelezwe kwenye mikoa mingine.

"Wafugaji wengine nchini wakiweza kutenga maeneo yao na kupewa mafunzo na kulima, itakuwa njia sahihi pia ya kuwasaidia wafugaji kuondokana na hali ya kuhamahama na mifugo yao kutafuta malisho," alisema Profesa Gabriel.

Aidha, alitoa wito kwa Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwilawa, kuhakikisha anashirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, kutunza mashamba hayo dhidi ya uvamizi wowote wa watu kufuata malisho hayo au kuingiza mifugo yao bila utaratibu unaokubalika.

Alisema lengo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha uwepo wa mifugo bora nchini ambayo inatokana na kula malisho bora ya kisayansi, badala ya kula wingi wa majani, wale majani yaliyo bora.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, aliiomba wizara hiyo kupitia kwa Katibu Mkuu, kusambaza wataalamu wake wa malisho katika maeneo mengine hapa nchini ili kuwashauri wakulima kuwa na mashamba mengi ya malisho bora ya mifugo, ambayo yatakuwa na tija kwa wafugaji kwa kuwa na mifugo bora.

Kijazi, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ina majosho 10 ya kuoshea mifugo huku akiishukuru wizara kwa kuwapatia fedha ya kukarabati majosho matatu na kuiomba wizara iwasaidie pia fedha nyingine kwa ajili ya kukarabari majosho saba yaliyobaki ili wafugaji wengi zaidi katika halmashauri hiyo waweze kuogesha mifugo yao.

Kuhusu idadi ya mifugo iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Kijazi alisema kuna mifugo takriban 600,000, ng'ombe wakiwa 350,000, mbuzi na kondoo zaidi ya 200,000, licha ya halmashauri kuwa na changamoto ya kutokuwa na machinjio nzuri.

Aliiomba wizara kutoa msaada wowote ili kuiwezesha halmashauri hiyo kuwa na machinjio nzuri na ya kisasa, kulingana na idadi ya mifugo iliyopo na hatimaye kuweza kuuza nyama ndani na nje ya nchi.

Akibainisha umuhimu wa uwepo wa mashamba bora ya malisho yanayotokana na kupandwa kwa aina mbalimbali za nyasi zilizofanyiwa utafiti wa kisanyansi na kuthibitishwa kuwa ni bora kwa malisho ya mifugo.

Ofisa Mifugo Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bezia Rwongezibwa, alisema wafugaji wanafundishwa kulima, kupalilia, kuweka mbolea, kuvuna na hatimaye kuhifadhi malisho hayo ambayo yatatumika wakati wa uhaba wa malisho.

Baadhi ya wananchi wakiwemo wa vikundi vya wajasiriamali ambao walijitolea kulima mashamba darasa kwa ajili ya mifugo kutoka katika Kijiji cha Mahambe, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, walisema wizara hiyo imewatia moyo namna ya kulima malisho na kuyahifadhi, ambapo baadhi yao wameanza kupanda malisho hayo ili wapate mifugo bora wakiwemo ng'ombe.

Walisema uwepo wa mashamba darasa katika eneo lao ni darasa tosha kwao kwa kuwa wataweza kujifunza zaidi kuhusu malisho bora ya mifugo na hatimaye kulima katika mashamba yao.




Scanned with CamScanner

kutenga maeneo yao na kupewa mafunzo

Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Kijazi

katika mashamba yao.

**UKAGUZI**



KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (anayeshughulikia mifugo) Profesa Elisante Ole Gabriel (kulia) akizungumza wakati alipokuwa akikagua Shamba Darasa la Malisho Mora ya Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu).

# Bwawa la Maji Nyumba ya Mungu lafurika zaidi ya uwezo wake

**Na GIFT MONGI,** *Mwanga*

BWAWA la Maji la Nyumba ya Mungu limejaa

jambo ambalo halijawahi kutokea zaidi ya miaka kumi huko nyuma,"alisema.

Katika hatua nyingine, Segule alisema walishachukua tahadhari kwa kutoa elimu

kali (TSN), Magnus Mahenge ali-

wake umeisha.

washukuru kwa kumchagua.

kuwa majumbani kwenye kipindi hiki shule zimefungwa .

SINGIDA

MTANZANIA UK 9

# Serikali yaanza mkakati wa malisho bora ya mifugo

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI imesema itahakikisha changamoto ya malisho ya mifugo nchini inatatuliwa kwa wafugaji kuelimishwa namna ya kulima malisho bora yenye tija kwa mifugo yao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel, wakati akikagua shamba darasa la malisho ya mifugo katika Kijiji cha Mahambe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida na kubainisha kuwa, serikali itaendelea kuwatia moyo wafugaji ili wawe na mashamba ya malisho bora ya mifugo yao. Licha ya hilo alisema kuwa pamoja na kuhakikisha uwepo wa maji ya kutosha ya kunyweshea mifugo mambo ambayo yatasaidia kudhibiti migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumaji wengine wa ardhi.

"Makatibu tawala wa mikoa mingine waige mfano wa Mkoa wa Singida kwa kuandaa mashamba ya malisho ya mifugo, lazima iendelezwe kwenye mikoa mingine. Wafugaji wengine nchini wakiweza kutenga maeneo yao na kupewa mafunzo na kulima malisho yao itakuwa njia sahihi pia ya kuwasaidia wafugaji kuondokana na hali ya kuhamahama ya mifugo yao kutafuta malisho," alisema Prof. Gabriel Aidha alitoa wito kwa Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwilawa kuhakikisha anashirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kutunza mashamba hayo dhidi ya uvamizi wowote wa watu kukata malisho hayo au kuingiza mifugo yao kulisha bila utaratibu unaokubalika.


Pia amewataka wafugaji kote nchini kufahamu nchi yeyote duniani inaendeshwa kwa sheria, taratibu na kanuni hivyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi haitamtetea mfugaji yeyote atakayeenda kinyume na sheria kwa kulisha mifugo yake katika eneo au shamba la mmiliki mwingine bila kufuata utaratibu.

Katibu mkuu huyo ameongeza kuwa lengo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha uwepo wa mifugo bora nchini ambayo inatokana na kula malisho bora ya kisayansi, ambapo badala ya kula wingi wa majani wale majani yaliyo bora.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi ameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel, kusambaza wataalam wake wa malisho katika maeneo mengine hapa nchini ili kuwashauri wakulima kuwa na mashamba mengi ya malisho bora ya mifugo ambayo yatakuwa na tija kwa wafugaji kwa kuwa na mifugo bora.

Scanned with CamScanner

MAJIRA UK 7.



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, akizungumza baada ya kukagua shambadarasa la malishobora ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, ambako alisema serikali itahakikisha kwamba changamoto za malisho ya mifugo nchini zinatatuliwa kwa kuelimisha wafugaji kuhusu namna ya kulima malisho bora yenye tija kwa mifugo yao.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

NIPASHE UK 10

# JKU yashauri wakazi Pemba kufuga samaki

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

KIASI cha kilo 209 za samaki aina ya mwatiko wenye thamani ya zaidi ya Sh. milion 1, zimevuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) katika kituo cha Muambe Mkoa wa Kusini Pemba, huku wakazi wa maeneo jirani wakishauriwa kujikita katika ufugaji wa kitoweo hicho.

Akizungumza baada ya uvuaji wa samaki hao, Mkuu wa kituo cha JKU Muambe, Kaptein Issa Bakar Othman, alieleza samaki waliovuliwa wamechukua miezi tisa tangu kuingizwa katika mabwawa yao wakiwa vifaranga.

Akizungumzia ushirikiano na wakazi walio pembezoni mwa kambi hiyo, Kaptein Issa alisema wanashirikiana vizuri katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Hapo awali tulipoanza kufanya mradi huu kulikuwa na tatizo la baadhi ya vijana wa maeneo ya karibu na kambi yetu kuvamia mabwawa yetu na kuharibu miundombinu pamoja na kuwavua samaki waliomo kwenye mabwawa, lakini baada ya kukaa na wazee wa kijiji na kuzungumza nao, tabia hiyo imeachwa," alisema Kaptein Issa.

Akitoa wito kwa jamii hasa wale ambao wanaishi karibu na bahari kuanzisha mradi wa ufugaji samaki, kwani una faida kubwa.

"Mradi huu una faida kubwa sana kwani ukizingatia kuwa hivi sasa kilo moja ya samaki ni kati ya shilingi 7,000 hadi 8,000," alisema.

Naye mtaalamu wa ufugaji samaki JKU Muambe, Sajent Bakari Hamad, alieleza kuwa changamoto kubwa ambazo wanakabiliana nazo katika mradi huo ni mabadiliko ya hali ya hewa ambapo muda mwingine maji ya bahari hayaingii inavyotakiwa.

Aidha, kufa kwa vifaranga au kuliwa na baadhi samaki ambao huwa wanapenya kutoka baharini na kuingia katika mabwawa yao.



# Bil. 3.2/- z

MWANANCHI UK 6.

# * Ikungi waja na mradi wa malisho ya mifugo *

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Katibu mkuu wa mifugo, Profesa Elisante ole Gabriel amesema Serikali imejipanga kutatua uhaba wa malisho ya mifugo nchini ili kuongeza ufanisi.

Mtendaji huyo amesema mkakati uliopo ni kuwaelimisha wafugaji namna ya kulima malisho bora yenye tija kwa mifugo.

Profesa Gabriel amesema alipokuwa akikagua shamba darasa la malisho katika Kijiji cha Mahambe wilayani Ikungi mkoani Singida.

"Hatua hii itasaidia kudhibiti migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumaji wengine. Makatibu tawala wa mikoa mingine waige mfano wa Singida wa kuandaa mashamba ya malisho," alisema.

Miradi ya kilimo cha malisho ya mifugo, katibu mkuu huyo alisema itawatia moyo wafugaji kuwa na mashamba yao hivyo kufuga kisasa na kuongeza tija.

"Wafugaji wakiweza kutenga maeneo kisha kupewa mafunzo na kulima malisho itawasaidia kuondokana na ufugaji wa kuhamahama kutafuta malisho," alisema Profesa Gabriel.

Mbali na hilo, alimtaka mkurugenzi wa utafiti, mafunzo na ugani wa wizara hiyo, Dk Angello Mwilawa kushirikiana na Halmashauri ya Ikungi kuyatunza mashamba hayo kwa kuzuia wafugaji kulisha mifugo yao kukata nyasi bila utaratibu unaokubalika.

Mkurugenzi wa Ikungi, Justice Kijazi aliomba wizara kupeleka wataalam wa malisho maeneo mengine nchini ili kuwashauri wakulima namna nzuri ya kumiliki mashamba ya malisho bora ya mifugo ili kuongeza tija kwa wafugaji.

Ufugaji ni miongoni mwa sekta zinazoajiri Watanzania wengi nchini lakini inakabiliwa na changamoto nyingi zinazosababisha migogoro ya mara kwa mara hivyo kupunguza tija.

Ikiwa ni ya tatu kwa wingi wa mifugo Afrika nyuma ya Ethiopia na Sudan kabla haijagawanyika, Tanzania inakabiliwa na uhaba wa malisho na maji unaosababisha mifugo kuingizwa kwenye mashamba ya wafugaji kwa ajili ya vyote viwili.

Kukabiliana na hilo, Serikali inawahamasisha wengi kupunguza idadi ya mifugo waliyonayo ili wafuge michache yeye tija kubwa zaidi.

**MALISHO**

**Katika kuhakikishaalisho yanapatikana, mamlaka zinajiwekea mikakati ya kuzalisha. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri) kituo cha Mpwapwa kinao mradi wa kuanza kufunga mbegu za malisho kuwaruhusu wafugaji kuzipanda popote nchini hivyo kutulia na kuweka makazi ya kudumu. Kituo hicho kinakusudia mbegu za malisho ziwe zinapatikana dukani kama zilivyo za mahindi au mazao mengine.**